JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WAKALA WA USAJILI UFILISI NA UDHAMINI**

**(RITA)**

# TAARIFA KWA UMMA

## KUANZA KWA ZOEZI LA UHAKIKI WA BODI ZA WADHAMINI

Ofisi ya Kabidhi Wasii Mkuu/ Msimamizi Mkuu wa Wadhamini inafanya zoezi la uhakiki wa Bodi za Wadhamini ilizosajili. Uhakiki utafanyika katika wilaya zote ambapo maafisa wa RITA watatembelea na kufanya ukaguzi huo utakaohusisha kutembelea Ofisi za Bodi hizi na kujiridhisha iwapo zinafanya shughuli zake kwa mujibu wa katiba zake. Bodi za wadhamini zinataarifiwa kuhakikisha nyaraka zote za taasisi zao zinapatikana wakati wa zoezi hili.

Viongozi wa taasisi zote zilizofutwa na orodha yake kuwekwa katika tovuti ya Wakala (www.rita.go.tz) wanapaswa kukabidhi vitu vifuatavyo katika Ofisi za Katibu Tawala wa Wilaya ambapo Bodi hizo zipo ndani ya siku 14 kuanzia tarehe ya tangazo hili. ;-

a) Cheti halisi cha usajili wa taasisi mlichopewa baada ya kusajiliwa **(Original Certificate).**

b) Orodha ya mali zote zilizokuwa zinamilikiwa na Taasisi husika. **(Hizi ni mali zinazohamishika na zisizohamishika)**

EMMY K. HUDSON

**KAIMU AFISA MTENDAJI MKUU/KABIDHI WASII MKUU.**